

# KiuFunza: Malipo ya walimu kulingana na utendaji

## 1. KiuFunza ni nini?

Malipo ya walimu kulingana na utendaji ni mfumo wa motisha unaounganisha malipo ya bakshishi kwa walimu na viwango vya ujuzi wanavyofikia wanafunzi wao katika kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK). KiuFunza – ni kifupi cha maneno ya Kiswahili **Kiu ya Kujifunza** – ni programu ambayo imekuwa ikitekeleza na kufanyia majaribio mfumo huu nchini Tanzania tangu mwaka 2013.

Kutokana na majaribio haya, walimu hulipwa kulingana na kiwango walichojifunza wanafunzi wao: kadri watoto wanavyomudu stadi za msingi za KKK darasani (kwa mujibu wa upimaji






Muhtasari huu umeandikwa na umeandaliwa na Twaweza East Africa.

S. L. P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
S: +255 22 266 4301 | B: info@twaweza.org |
www.twaweza.org/sauti



Twaweza ni sisi

huru unaofanywa), ndivyo bakshishi ya mwalimu husika inavyongezeka. Bakshishi ya utendaji kazi inalipwa kama nyongeza kwenye mshahara wa mwalimu, hivyo, haihatarishi mishahara iliyopo. Mfumo wa KiuFunza unawalenga walimu wa Darasa la I, II na III, kwa sababu walimu hawa ndio wenye wajibu wa kufundisha KKK na wana madarasa yenye wanafunzi wengi zaidi.





Wazo la malipo kulingana na utendaji ni rahisi. Kilicho muhimu katika elimu ni *kuona watoto wanajifunza*. Sababu mojawapo ya walimu kukosa motisha na ari ya kufanya kazi, kutafuta kazi nyingine na utoro shuleni - ni **Motisha.** KiuFunza inatumia motisha yenye nguvu (fedha) kuiunganisha na matokeo ya kujifunza.

Muundo wa KiuFunza ni rahisi pia: mwanzoni mwa mwaka wa masomo, wafanyakazi wa programu ya KiuFunza hutembelea shule, kuwaeleza walimu kuhusu ofa ya bakshishi na kuandikisha walimu watakaoshiriki; mwishoni mwa mwaka wa masomo, wanafunzi wanapimwa kuona viwango vya ujuzi waliopata; kwa kuangalia alama za majaribio walizopata wanafunzi, malipo yanakokotolewa na motisha hutolewa kwa mwalimu husika mwanzoni mwa mwaka ujao. Muhimu zaidi, shule na wasimamizi hupokea ripoti ya ufaulu wa wanafunzi kulingana na somo na darasa husika ili kuwasaidia kutambua mapungufu na kuboresha ufundishaji wao.

KiuFunza **haitoi mafunzo ya ualimu wala msaada wowote wa ziada** kwa walimu ili kuwasaidia kufaidika na ofa ya motisha. Badala yake KiuFunza **inalenga kutoa motisha** ya walimu pekee, siyo uwezo wao wa kufundisha au fursa za kutoa elimu bora.

## 2. KiuFunza imepata mafanikio gani?

Motisha ya KiuFunza imelipwa miaka ya hivi karibuni (2019-2021) kwa walimu katika mikoa iliyowekewa alama nyekundu na kijani kwenye ramani. Wilaya za mikoa ya Kigoma na Tanga (kijani) pia zilikuwa sehemu ya awamu za mwanzo za KiuFunza (2013-2016), pamoja na wilaya zilizowekwa alama ya bluu. Kwa kila awamu, mikoa na wilaya hizo zilichaguliwa kinasibu kutoka orodha ya mikoa yote nchini na wilaya zote za mikoa hiyo. Kila mkoa, wilaya na shule Tanzania Bara ilikuwa na sifa ya kuwa sehemu ya KiuFunza.




Katika awamu tatu za utekelezaji kati ya mwaka 2013 na 2021, KiuFunza imelipa bakshishi yenye thamani ya shilingi bilioni 1.6 (tazama Jedwali la 1). Kwa miaka hiyo, malipo yametolewa kwa walimu 5,660 (baadhi ya walimu walipokea malipo kwa zaidi ya mwaka mmoja). Motisha hii ya nyongeza na jitihada za walimu zimesaidia kuboresha matokeo ya kujifunza kwa wanafunzi 250,175 kwa miaka ya utekelezaji[1].

Wastani wa bakshishi kwa kila mwalimu ni asilimia 3.5 ya wastani wa mshahara wa mwaka mzima wa mwalimu. Kwakuwa hii ni bakshishi inayoangalia utendaji, walimu wengine hupata fedha zaidi

1 Jumla ni "miaka ya mwanafunzi", siyo mwanafunzi mmoja mmoja, maana baadhi ya wanafunzi wako kwenye program kwa zaidi ya mwaka mmoja.

ya wastani na wengine pungufu ya wastani. Kiasi cha malipo ya bakshishi hutegemea mwalimu anafundisha wanafunzi wangapi, na wanafunzi hao wamefaulu kwa kiwango gani majaribio ya KKK ya KiuFunza.


| KiuFunza-<br>Malipo ya Fedha<br>kulingana na utendaji | Wanafunzi walengwa | Walimu waliolipwa | Fedha za bakshishi<br>walizopata<br>Sh |
|---|---|---|---|
| **JUMLA** | **250,175** | **5,660** | **1,615,459,040** |
| **Kwa Mwaka** | | | |
| **2021** | **26,751** | **547** | **204,000,000** |
| **2020** | **27,777** | **534** | **204,000,000** |
| **2019** | **27,463** | **560** | **204,000,000** |
| **2016** | **48,064** | **922** | **251,827,040** |
| **2015** | **36,701** | **892** | **315,000,000** |
| **2014** | **42,706** | **1,124** | **237,492,000** |
| **2013** | **40,713** | **1,081** | **199,140,000** |

## 3. KiuFunza imeleta matokeo gani kwenye ujifunzaji wa wanafunzi?

Programu ya KiuFunza imekuwa mada kwenye tathmini makini mbalimbali za matokeo ya kujifunza, zinazotekelezwa na watafiti huru wanaoshirikiana na Abdul Latif Jameel Poverty Action Lab (J-PAL). Tathmini hizi za matokeo zinaonesha kuwa awamu zote za KiuFunza ziliboresha ujifunzaji wa wanafunzi, lakini jambo tulilojifunza ni kuhusu jinsi gani ya kubuni na kutekeleza vizuri programu hii ya motisha. Baada ya kujaribu mbinu kadhaa za kutoa motisha, mbinu yenye tija zaidi na gharama nafuu zaidi iligunduliwa kuwa nzuri tuliiita jina la Stadi (Lipa ujuzi): hii ni mbinu mpya ya kupima ujuzi, iliyoandaliwa na kufanyiwa majaribio kwa mara ya kwanza nchini Tanzania mwaka 2015-16, ikiwa na bakshishi inayotolewa kwa kufuata ujuzi wa vipengele vya mtaala. (kwa mfano, kusoma sentensi chache, hesabu za kutoa). Mbinu hii kwasasa inatumika kwenye programu nzima ya KiuFunza.

Utafiti wa matokeo uligundua kuwa mfumo wa kutoa zawadi kwa Stadi mwaka 2015-16 ulichangia kuboresha ujifunzaji wa wanafunzi sawa na **miezi mitatu ya ziada ya masomo** kwa gharama ya chini ya mshahara wa mwezi mmoja. Kwahiyo, KiuFunza inatoa thamani ya fedha ikilinganishwa na programu nyingine zinazotoa msaada kama vile kuongeza vitabu au kutoa mafunzo kwa walimu.


Hivi karibuni, motisha za KiuFunza zimesababisha maboresho makubwa ya matokeo ya ujifunzaji katika awamu zote, na kwenye stadi zote za KKK. Grafu ifuatayo hapa chini inaonesha hili kwa ujuzi wa hesabu za darasa la 3 mwaka 2021, lakini madarasa na ujuzi mwingine unaonesha matokeo sawa. Jedwali linaonesha kuwa wanafunzi katika shule "zenye mradi" wa KiuFunza wanafanya vizuri katika stadi zote zilizopimwa, lakini wanafanya vizuri zaidi kwenye stadi kuu za motisha za kujumlisha na kutoa. KiuFunza pia inaboresha viwango vya ufaulu kwenye stadi ngumu kama kuzidisha na kugawanya.




Makadirio ya awali yanaonesha kuwa uboreshaji uliochangiwa na jitihada za KiuFunza kwenye kuongeza ufaulu ni sawa na theluthi moja ya ujifunzaji kwa mwaka wa masomo. Hivyo, theluthi moja ya mwaka wa masomo huongezwa kwenye kile ambacho kwa kawaida mwanafunzi hujifunza. Utafiti unaonesha zaidi kuwa wanafunzi wasiofanya vizuri wananufaika zaidi na programu ya KiuFunza.

### 4. Walimu wanasemaje kuhusu malipo kulingana na utendaji?

Timu za utafiti ziliuliza maoni ya walimu kuhusu malipo kulingana na utendaji. Matokeo ya maoni yao yamebaki vilevile kwa miaka mingi: walimu wanapenda malipo kulingana na utendaji wao na matokeo. Takribani walimu wote wa masomo husika wanaunga mkono wazo la kutoa bakshishi zinazotokana na mafanikio ya wanafunzi kwenye majaribio ya kujifunza. Na walimu wengi hupendelea zaidi malipo ya nyongeza kama haya ya motisha kulingana na utendaji kazi kuliko nyongeza ya malipo ya jumla kwa wote.



Kwa ujumla walimu wanahisi wana mzigo mkubwa wa kazi na hawathaminiwi ipasavyo. Lakini malipo kulingana na utendaji yanawapa motisha kubwa. Inaonesha kuwa mfumo huu wa malipo unajali wanachofanya walimu. Kwenye utafiti wa ubora na viwango, walimu waliulizwa waseme wanajisikiaje wanapokuwa kwenye shule yenye mradi wa KiuFunza. Baadhi ya kauli zao zimeoneshwa kwenye mchoro hapa chini.




## 5. Kwanini malipo kulingana na utendaji ni jambo muhimu kufanya?

Tanzania imefanya vizuri sana kwenye uandikishaji wa wanafunzi shuleni. Tunahitaji kuendeleza mafanikio makubwa ya uandikishaji kwa kujielekeza kuboresha ujifunzaji na motisha kwa walimu. Hii ni muhimu hasa katika madarasa ya mwanzoni (darasa la I, II na III). Katika ngazi hizi stadi na ujuzi lazima vifundishwe kikamilifu kama msingi wa ujifunzaji wote wa siku zijazo – Endapo watoto watakosa ujuzi huu wana nafasi ndogo ya kufanya vizuri huko mbeleni.

Walimu wenye motisha na waliotiwa hamasa ndio tegemeo kwenye kufanikisha hili, lakini ukubwa wa madarasa unaoongezeka umebaki kuwa changamoto ya kila siku. Changamoto hii ni kubwa zaidi hasa madarasa ya I, II na III ambapo ujuzi wa msingi unatakiwa kufundishwa ipasavyo na wanafunzi wajifunze kikamilifu. Ukubwa wa madarasa utaendelea kuongezeka, siyo kupungua kwa miaka ijayo. Kulipa bakshishi kwa kila mwanafunzi anayepata ujuzi fulani hubadilisha changamoto hii na kutoa fursa kwa mwalimu: walimu wanaweza kupata bakshishi kubwa zaidi kama watafundisha watoto wengi zaidi. Walimu sasa wanakuwa wamiliki wa mafanikio yao wenyewe, wakitambuliwa rasmi jitihada zao na kupata fedha kulingana na juhudi

zao. Ushahidi wa kitafiti unaonesha kwamba motisha ya aina hii inajenga jumuiya ya shule yenye ari na inayojituma kufanya kazi.

Malipo kulingana na utendaji yana faida zifuatazo, ikilinganishwa na mageuzi au mbinu nyingine:

- Wazo ni rahisi na linaeleweka kiurahisi kwa walimu, ambao ni walengwa wakuu.
- Malipo kulingana na utendaji kazi hayahitaji walimu kufanya lolote isipokuwa kujikita katika kuboresha matokeo kujifunza kwa somo husika.
- Hakuna mafunzo ya ualimu (ingawa malipo ya utendaji na mafunzo ya KKK vinaweza kusaidiana).
- Walimu na shule zilizofaulu zaidi ni zile zinazojipanga kibunifu ili kuboresha ujifunzaji.

## 6. Msaada wa Serikali kwa KiuFunza

Twaweza imeungwa mkono na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu mwanzo wa KiuFunza. Mwaka 2013, programu hii ilizinduliwa na aliyekuwa Waziri wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Hawa Ghasia. Mwaka 2014, Naibu Waziri wa wakati huo, Kassim Majaliwa (sasa Waziri Mkuu) alitembelea shule za KiuFunza jijini Dar es Salaam. Baada ya kuona ufanisi wa KiuFunza, mwaka 2017, Waziri wa TAMISEMI, George Simbachawene aliitaka Twaweza kubuni mpango wa malipo ya ufaulu ambao unaweza kuongezwa ili kuwanufaisha wanafunzi, walimu na shule zaidi. Kwa maneno yake:

*“Unaweza kumlipa mwalimu shilingi milioni 10 kama mshahara wake na atakuambia kwa uwazi kabisa kwanini haitoshi. Lakini unapompa mwalimu huyo huyo laki moja kama bakshishi ya ufaulu wao, utawatia moyo wa kufanya zaidi na zaidi.”*

Msaada huu wa serikali umesababisha kufanyika kwa utekelezaji wa awamu ya mwisho wa KiuFunza kwenye mikoa sita kati ya mwaka 2019 na 2022 (KiuFunza III). Katika awamu hii, Maafisa wa Udhibiti Ubora wa Shule walikuwa sehemu ya timu za utekelezaji za KiuFunza. Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilitoa msaada wa aina mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ushauri wa kubuni, takwimu na kibali cha kuzifikia shule za mradi. Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) lilipitia na kutoa ushauri kuhusu upimaji wa wanafunzi.

## 7. Hitimisho

Kuna hoja tatu zenye nguvu za kuboresha ujifunzaji wa wanafunzi kupitia motisha ya walimu. Kwanza, tafiti za kisayansi za hivi karibuni zinaonesha kuwa watoto wanaosoma shule zenye mpango wa malipo kulingana na utendaji **hujifunza zaidi stadi muhimu za KKK**. Tafiti hizi zilifanyika nchini Tanzania na zililinganisha ujifunzaji wa wanafunzi katika sampuli kubwa yenye uwakilishi wa shule za msingi za umma zenye bakshishi ya ufaulu dhidi ya zile zisizo na bakshishi. Mbinu hii ni muhimu, kwasababu ufaulu wa majaribio ni kielelezo kizuri cha mafanikio ya mwanafunzi shuleni na maishani mwake siku zijazo.

Pili, malipo kulingana na utendaji yana **manufaa makubwa yenye gharama ndogo**: yanachangia kuboresha ujifunzaji kwa kila shilingi moja ya Tanzania inayotumika kuliko programu nyingine nyingi zilizofanyiwa majaribio duniani kote. Programu hizo nyingine zilizofanyiwa majaribio ni

pamoja na; a) kupeleka ruzuku ya kila mwanafunzi shuleni, b) kupunguza ukubwa wa darasa, c) kugawa vitabu, kompyuta mpakato au vifaa vingine shuleni, au d) kuwapa walimu mrejesho kuhusu ufundishaji wao bila motisha yoyote.

Tatu, malipo kulingana na utendaji kazi ni **kichocheo chenye nguvu** katika kuleta tija kwenye matumizi makubwa ya fedha yaliyopo kwenye mfumo wa elimu kama vile mishahara ya walimu na ruzuku za uendeshaji wa shule. Malipo kulingana na utendaji hufanya matumizi haya kuwa na tija katika kuboresha stadi na ujuzi wa wanafunzi.

Katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, KiuFunza imeanzisha na kuendesha mfumo rahisi na wenye ufanisi wa malipo ya walimu kulingana na utendaji nchini Tanzania, ambao ni mfumo wa kwanza wa aina yake duniani. Utafiti huru umeonesha kuwa mpango huu wa motisha ya utendaji kazi umepandisha viwango vya ujifunzaji kwa wanafunzi wote wa madarasa ya chini, wakiwemo wanafunzi waliokuwa wanafanya vibaya.

KiuFunza kwa sasa inafanya kazi kwenye maeneo machache hapa nchini kwa kushirikiana na serikali. Awamu mpya itazilenga shule dhaifu zaidi kwenye wilaya nyingi zaidi.

